



ASb  
approved




Kiswahili

# Bibi, Sungura na Tembo


Brigid Simiyu  
Marleen Visser



Bibi alianza,  
“Sungura na  
Tembo walikuwa  
marafiki tena  
majirani.”



Sungura alipenda  
uyoga lakini  
alikuwa mvivu  
sana. Hakulima.




Sungura hakupata  
uyoga.

Alianza kuiba ndizi  
za Tembo.



Tembo aliimba,  
“Nitamshika  
mwizi!”

Sungura aliogopa.



Kima alimchungia  
Tembo shamba  
lake.

Lakini, Sungura  
hakuiba.



Tembo alienda  
kutazama.

Sungura alijificha  
ndani ya matawi  
ya maboga.



Tembo aliangalia  
kila mahali.


Hakumpata mwizi.



Siku nyingine,  
Sungura alijificha  
ndani ya boga  
kubwa.



Tembo aliliona hilo  
boga kubwa  
akalimeza.




Boga lilisonga  
tumboni mwa  
Tembo.



Tembo alilitema  
boga.

Sungura alitoka  
ndani akatoroka.



Bibi alisema, “Na huo ndio mwisho wa hadithi.”

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

## Bibi, Sungura na Tembo

Author - Mutai Chepkoech

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Marleen Visser

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)